

**MKATABA WA KUPANGISHA PANGO LA BIASHARA
KATIKA SHAMBA NA. 38 MNY/4633
KIJIJI CHA ILUCHA
WILAYA YA MANYONI**

KATI YA

HOSIANA KUSIGA

(MPANGISHAJI)

NA

YUHO AGROPROCESSING INDUSTRIES

(MPANGAJI)

KWA UPANGISHAJI WA PANGO LA BIASHARA

**MKATABA WA KUPANGISHA PANGO LA BIASHARA
KATIKA SHAMBA NA. 38 MNY/4633
KIJIJI CHA ILUCHA
WILAYA YA MANYONI**

KATI YA

HOSIANA KUSIGA

(MPANGISHAJI)

NA

YUHO AGROPROCESSING INDUSTRIES

(MPANGAJI)

KWA UPANGISHAJI WA PANGO LA BIASHARA

MKATABA WA KUPANGISHA PANGO LA BIASHARA

Mkataba huu umesainiwa leo hii tarehe 29 Mwezi Julai Mwaka 2021.

KATI YA

HOSIANA KUSIGA wa S.L.P 6366 Mwanza, (ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MPANGISHAJI**", (jina ambalo litawahusisha warithi wake, wawakilishi, ndugu na jamaa zake) wa upande mmoja;

NA

YUHO AGROPROCESSING INDUSTRIES wa S.L.P 6366 Mwanza (ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MPANGAJI**")

KWA KUWA, Mpangishaji ni mmiliki halali wa pango kama ilivyoainishwa kwenye vielelezo halali na kuhakikiwa na mpangaji, na

KWA KUWA, Mpangishaji ana nia ya kupangisha pango hilo kwa ajili ya biashara kwa mpangaji, na Mpangaji ameonyesha nia ya kutaka kupangisha pango hilo la biashara kwa malipo ya kodi na masharti mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu;

HIVYO BASI, MKATABA huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:-

1. **KWAMBA**, mkataba huu ni wa kipindi cha miaka kumi (10) na utakua ukifanyiwa mapitio kadri hali itakapolazimu ili kukidhi haja ya mabadiliko ya muda.
2. **KWAMBA**, miaka kumi (10) kama ilivyobainishwa kwenye aya ya kwanza hapo juu itanza kuhesabiwa kuanzia Tarehe 29 Mwezi Julai, 2021.
3. **KWAMBA**, mpangaji atakua akilipa kiasi cha shilingi laki tatu tu za kitanzania (Tsh 300,000/=) kama kodi ya pango kwa mwezi.

4. **KWAMBA**, mpangaji ili kusaini mkataba huu atapaswa kulipa kodi ya miaka mitatu yaani kiasi cha shilingi milioni kumi na elfu themanini tu za kitanzania (Tsh 10,080,000/=) kama malipo ya awali ya mkataba huu.
5. **KWAMBA**, mpangaji hatoruhusiwa kumpangisha mtu mwingine pango hilo la biashara bila idhini ya mpangishaji.
6. **KWAMBA**, mpangaji anatakiwa kutunza pango hilo la biashara na mazingira yake katika hali ya usafi.
7. **KWAMBA**, mpangaji atawajibika kulipa bili zote za maji na umeme kwa kipindi chote cha mkataba huu.
8. **KWAMBA**, mpangaji atapaswa kutoa taarifa ya maandishi miezi mitatu kabla ya kikomo cha mkataba huu iwapo atapenda kuendelea na kipindi kingine cha upangaji.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa saini na Mpangishaji na Mpangaji mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

UMETIWA SAINI na KUTOLEWA

na **HOSIANA KUSIGA** ambaye ninamfahamu/
ametambulishwa kwangu na.....
ambaye namfahamu leo hii tarehe...09...Mwezi
Tulai..... Mwaka 2021.

.....
MPANGISHAJI


Mbele ya:-

Jina: Johnpaul Nicholas Kaunara

Wadhifa:

Saini:

Tarehe: 09/08/2021



IMETIWA LAKIRI YA YUHO
AGROPROCESSING INDUSTRIES

LTD ambaye ninamfahamu/
ametambulishwa kwangu na

.....
ambaye namfahamu leo hii tarehe.....²⁹Mwezi
...⁰⁷.....Mwaka 2021.



[Signature]
.....
MPANGAJI

Mbele ya:-

1. Jina: HOSIANA KUSIGA
Wadhifa: MKURUGENZI
Saini: [Signature]
Tarehe: 29.07.2021

2. Jina: YUSTER Z. BYABUSAA
Wadhifa: MKURUGENZI
Saini: [Signature]
Tarehe: 29.7.2021